**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI**
**(EWURA)**

**NAMBA YA MALALAMIKO: GA.71/472/WZ/2024/10**
**NAMBA YA LOIS: COMP 2024 - 00000268**

**KATI YA**

**JACKSON BENGUYE NTUYAMALE..................................................MLALAMIKAJI**

**NA**

**MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA**
**KASULU (KASULU WSSA) ............................................................ MLALAMIKIWA**

---

# TUZO YA MAKUBALIANO

---

***(Imetolewa na Kamati ya Sheria na Utawala ya Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA katika kikao chake cha 146 cha tarehe 17 mwezi Machi 2025)***

## 1. Maelezo ya Awali

Mnamo tarehe 22 Novemba 2024, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji "EWURA" ("Mamlaka") ilipokea malalamiko kutoka kwa Bw. Jackson Benguye Ntuyamale wa Mtaa wa Nyumbigwa "B" Wilaya ya Kasulu Mkoa wa Kigoma, ("Mlalamikaji") dhidi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kasulu (Kasulu WSSA) ("Mlalamikiwa"). Mlalamikaji anamtaka Mlalamikiwa kurejesha huduma ya majisafi aliyokata mwezi Juni 2024, pamoja na kufuta deni la kiasi cha TZS 500,000/= kama tozo anayomdai Mlalamikaji ya kujiunganishia maji kinyume na taratibu.

Mlalamikaji anaeleza kwamba, aliunganishiwa huduma ya maji na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kasulu mnamo mwezi Februari 2024, kutoka kuwa mteja wa RUWASA ambapo awali walikua wanatoa huduma eneo hilo wanaloishi. Mlalamikaji anaeleza zaidi kuwa kwa kipindi cha miezi mitatu yaani mwezi Februari, Machi mpaka Aprili 2024, hakuwahi kupewa ankara ya maji.

Na ilipofika mwezi Mei 2024 alipewa ankara yenye deni la kiasi cha Shilingi 47,571/= ambapo alilipa deni hili kwa awamu nne kati ya tarehe 12 Juni 2024 mpaka tarehe 15 Juni 2024, alipomaliza ulipaji wa deni na kubakiwa na ziada ya kisha cha Shilingi 129.

Mlalamikaji anaeleza kuwa maofisa wa Mlalamikiwa walifika na kumkatia maji katika eneo lake tarehe 16 Juni 2024, ilhali alikua ameshamaliza kulipa deni lake lote. Baada ya kukatiwa maji alipokea barua kutoka ofisi ya Mlalamikiwa ikimtaka afike ofisini ili wajadili suala la yeye kurejeshewa huduma ambapo alifika mara kadhaa na hakuweza kupata ushirikiano kama alivyoahidiwa, na ilipofika tarehe 13 Agosti 2024 alikabidhiwa barua yenye deni la Shilingi 500,000/= na kuelezwa kuwa ni faini ya kujiunganishia huduma bila kufuata taratibu (Wizi wa maji).

Mlalamikaji alifanya jitihada za kutafuta haki ikiwa ni pamoja na kufika katika ofisi ya Katibu Tawala Wilaya ya Kasulu, ofisi ya Mkuu wa Wilaya Kasulu ambako hakupata suluhu. Mlalamikaji anaeleza zaidi kuwa aliamua kuwasilisha malalamiko yake katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kigoma, ambapo alielekezwa kuwasilisha malalamiko yake EWURA kwa utatuzi. Mlalamikaji aliwasilisha rasmi alalamiko yake kwa Mamlaka (EWURA) na kuiomba Mamlaka kumuamuru Mlalamikiwa kumrejeshea huduma ya maji na kufuta deni la Shilingi 500,000/= katika akaunti yake.

Malalamiko yalipokelewa ofisi za EWURA Kanda ya Magharibi tarehe 22 Novemba 2024. Baada ya kupokea malalamiko, tarehe 29 Novemba 2024, Mamlaka (EWURA), ilimwandikia Mlalamikiwa na kumuamuru kuwasilisha utetezi wake kwa maandishi ndani ya siku ishirini na moja (21) kwa mujibu wa Kanuni ya 6 (1) na 7 (1) ya Kanuni za EWURA za Utatuzi wa Migogoro TS Na. 428/2020.

Mlalamikiwa aliwasilisha utetezi wake tarehe 30 Disemba 2024, na kuieleza Mamlaka kwamba, walifanya ukaguzi wa wadaiwa sugu wa madeni ya ankara za maji mnamo tarehe 5 Juni 2024, lengo ikiwa ni ukusanyaji wa mapato, ambapo walikata huduma ya maji nyumbani kwa Mlalamikaji kutokana na deni la Shilingi 47,571/= lililotokana na malimbikizo ya ankara za miezi mitatu mfululizo.

Mnamo tarehe 9 Juni 2024, walipata taarifa kwamba Mlalamikaji amejiunganishia huduma ya maji baada ya kukatiwa huduma, hivyo walichukua hatua ya kukata maji kwa mara ya pili kuzuia upotevu, kumwandikia barua ya wito wa kumtaka alipe fidia ya wizi wa maji ya kiasi cha Shilingi 500,000/= ikiwa ni pamoja na kuomba msaada kituo cha polisi kusaidia zoezi la ukusanyaji madeni.

Kikao cha usuluhishi kati ya Wadaawa kilifanyika tarehe 28 Januari 2025, katika ukumbi wa mikutano wa hoteli ya Glowness Mtabila iliyoko Wilayani Kasulu. Mwisho wa kikao cha usuluhishi, pande zote mbili zilikubaliana kwamba

**(a)** Mlalamikaji atalipa kiasi cha Shilingi laki mbili (200,000/=) kufidia upotevu wa maji yaliyopotea kwa utaratibu ufuatao:

**(b)** Kiasi cha Shilingi laki moja (100,000/=) kitalipwa kufikia Jumamosi tarehe 1 Februari 2025.

**(c)** Kiasi kinachobaki cha Shilingi laki moja (100,000/=), kitalipwa kufikia tarehe 1 Machi 2025.

**(d)** Mlalamikiwa atarejesha huduma ya maji nyumbani kwa Mlalamikaji siku ya Jumamosi tarehe 1 Februari 2025, mara baada ya kuthibitisha kupokea malipo ya kiasi cha Shilingi laki moja (100,000/=) kama malipo ya awali kwa mujibu wa makubaliano, tajwa hapo juu.

Makubaliano haya yamefupishwa kimaandishi kama inavyoainishwa kwenye Kanuni ya 14 (4) ya Taratibu za Utatuzi wa Migogoro na kama inavyoainishwa kwenye fomu ya makubaliano.

## 2. <u>Makubaliano</u>

Pande zote mbili zimefikia muafaka kwamba;

**(e)** Mlalamikaji atalipa kiasi cha Shilingi laki mbili (200,000/=) kufidia upotevu wa maji yaliyopotea kwa utaratibu ufuatao:

(f) Kiasi cha Shilingi laki moja (100,000/=) kitalipwa kufikia Jumamosi tarehe 1 Februari 2025.

(g) Kiasi kinachobaki cha Shilingi laki moja (100,000/=), kitalipwa kufikia tarehe 1 Machi 2025.

(h) Mlalamikiwa atarejesha huduma ya maji nyumbani kwa Mlalamikaji siku ya Jumamosi tarehe 1 Februari 2025, mara baada ya kuthibitisha kupokea malipo ya kiasi cha Shilingi laki moja (100,000/=) kama malipo ya awali kwa mujibu wa makubaliano.hapo juu.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 14 (5) ya Taratibu za Utatuzi wa Migogoro makubaliano haya yameandikishwa kama Tuzo ya Mamlaka. Kila pande itabeba gharama zake katika shauri hili.

**IMETOLEWA KWA LAKIRI** ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) hapa Dodoma leo tarehe 17 mwezi Machi 2025.

..................................

**TONI S. MBILINYI**
**KATIBU WA BODI**